



WWF *for a living planet*

TANGAZO KWA UMMA

Maoni ya Wadau wa Umma juu ya Rasimu ya Taifa ya Viwango vya Uthibitishaji wa Misitu (National Forest Stewardship Standards - NFSS)

Tanzania imekuwa katika mchakato wa kuendeleza rasimu ya taifa ya Viwango vya uthibitishaji wa misitu (National Forest Stewardship Standards - NFSS) kulingana na mfumo wa uhakiki wa Baraza la Uthibitishaji wa Misitu la Kimataifa (Forest Stewardship Council – FSC). Kamati ya Kutengeneza Viwango (Standard Development Group - SDG), iliwasilisha maombi kwa Baraza la Uthibitishaji wa Misitu la Kimataifa (FSC), kuhusu dhamira ya kuandika Viwango vya uthibitishaji wa Misitu (NFSS).

Maombi hayo yalipitishwa mwaka 2015. Kamati ya Kutengeneza Viwango (SDG) imekamilisha uandikaji wa viwango hivyo kwa msaada mkubwa kutoka World Wide Fund for Nature - (WWF) ofisi ya Tanzania pamoja na msaada wa kiufundi na kifedha kutoka ofisi ya Kanda ya Afrika Mashariki (FSC Regional Office). Rasimu ya kwanza ilikamilika toka mwezi Mei 2016.

Mwezi Juni 2016, Rasimu ya pili ya Viwango vya uthibitishaji wa misitu (NFSS) ilifanyiwa majaribio katika mashamba makubwa ya miti yaliyopo Mafinga, Iringa na Misitu ya asili ina **yosimamiwa** na vijiji, iliyopo Kilwa, mkoani Lindi. Rasimu ya tatu imekamilika na ipo tayari kwa ajili ya kupata maoni kutoka kwa wadau wote nchini.

Mchakato wa kupata maoni kutoka kwa wadau kwa ajili ya Viwango vya uthibitishaji wa misitu (NFSS) utachukua muda wa siku 60 na zoezi litafanyika kati ya mwezi **Agosti tarehe 15 na mwezi Oktoba tarehe 15 mwaka 2016**. Kamati ya Kutengeneza Viwango (SDG) inawaalika umma na wadau wote wanaoguswa moja kwa moja kupitia rasimu hii, kuangalia ubora wa Viwango hivi katika kuchangia usimamizi endelevu na uwajibikaji wa uhifadhi msitu. Wadau wanaombwa kutoa maoni yao ambayo yatajumuishwa katika mchakato wa mwisho utakaofanywa na Baraza la Uthibitishaji wa Misitu la Kimataifa (Forest Stewardship Council – FSC), nakupitisha viwango hivyo ilivitumike popote pale Tanzania Bara.

Kwa ajili ya kupata seti kamili ya Viwango vya uthibitishaji wa Misitu vya taifa (NFSS), Tafadhali wasiliana na: [Isaac Malugu](mailto:imalugu@wwftz.org) kupitia Barua pepe (Email): imalugu@wwftz.org ; au tembelea [tovuti zifuatazo:](#)

<http://www.tafmp.co.tz>; [http://wwf.panda.org/who we are/wwf offices/tanzania](http://wwf.panda.org/who_we_are/wwf_offices/tanzania);

www.facebook.com/wwftanzania; www.twitter.com/wwftanzania;

www.mpingoconservation.org; www.mjumita.org; www.tnrf.org